

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



Maswali

1. Mfalme Nebukadreza alitengeneza nini?
2. Mfalme Nebukadreza aliamrisha eti nini?
3. Mbona Shadraka, Meshaki na Abednego waliogopa?
4. Waliamua kufanya nini?
5. Nini ilifanyika muziki ulipochezwa?
6. Mbona Mfalme Nebukadreza alikasirika?
7. Shadraka, Meshaki na Abednego waliadhibiwa namna gani?
8. Mfalme Nebukadreza aliona nini katika tanuru ya moto?
9. Shadraka, Meshaki na Abednego waliokoka namna gani kutoka kwa tanuru ya moto?
10. Mfalme Nebukadreza aliamrisha nini?

Majibu

1. Mfalme Nebukadreza alitengeneza sanamu kubwa ya dhahabu.
2. Kila mtu lazima ainame naaabudu sanamu ya dhahabu.
3. Mungu aliamru kwamba wasiinamie wala kuabudu kitu chochote.
4. Waliamua kutii Mungu hata kama ni kukufa.
5. Kila mtu aliinama chini isipokua Shadraka, Meshaki na Abednego.
6. Nebukadreza alikasirika kwa sababu wale marafiki 3 walikataa kumtii.
7. Shadraka, Meshaki na Abednego walitupwa ndani ya tanuru ya moto.
8. Nebukadreza aliona watu 4 wakitembea ndani ya tanuru.

Hawakuchomeka.

9. Mungu alituma malaika kuwaokoa kutoka kwa moto.
10. Mtu yejote asizungumze kinyume kwa Mungu wa kweli, aliye na uwezo juu moto.

82 Tanuru ya Moto

Kwa Biblia

Danieli mlango wa 3

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anauwezo juu hali zote. Anaweza kuokoa watu kutoka kwa kifo. Mungu husaidia wale wanaompenda na kumtii

Somo


Mfalme Nebukadreza alitengeneza sanamu. Hiyo sanamu ilikuwa kubwa sana. Ilikuwa na urefu wa mita 30 na upana wa mita 3. Sanamu ilitengenezwa kwa dhahabu. Nebukadreza aliiweka pahali tambarare karibu na Babeli.

Mfalme Nebukadreza alituma wajumbe kwa ufalme wake wote. Alituma wajumbe kwa manaibu, wakuu wake na wasimamizi wa wilaya zote. Mfalme Nebukadreza aliwaamrisha waje Babeli kwa sherehe maalum ya sanamu aliyokuwa ametengeneza.

Watu wengi walikuja kutoka pande zote za ufalme huo. Walikusanya kuangalia hiyo sanamu ya dhahabu ya ajabu yenye mfalme alikuwa ametengeneza. Mfalme Nebukadreza alisema kwamba lazima kila mtu aabudu hiyo sanamu ya dhahabu. Alisema wakati muziki ukichezwa, lazima kila mtu ainame naaabudu hiyo sanamu ya dhahabu. Yeyote atakayekataa kuinama na kuabudu sanamu, atatupwa ndani ya tanuru ya moto.

Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa marafiki wa Danieli. Walikuwa wameletwa kutoka Yuda kama watumwa. Waliabudu Mungu. Walifanya kazi na Danieli. Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa watu wa hekima. Walikuwa baadhi ya viongozi wa Babeli. Waliamrishwa kuenda kwa hiyo sherehe ya sanamu ya dhahabu. Waliamrishwa kuinama na waabudu hiyo sanamu.

Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa na uoga. Mfalme alikuwa ameamrisha wainame na waabudu sanamu ya dhahabu. Lakini Mungu alikuwa ameamrisha wasiabudu sanamu wala miungu.  Soma Kutoka 20:2-5. Pamoja walizungumzia hiyo shida. Waliomba Mungu. Waliamua kwamba lazima watii Mungu.



Kila mtu alikuja na kukusanyika kwa sababu ya sherehe maalum. Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa kwa huo umati wa watu. Mfalme Nebukadreza aliamrisha watu, "Muziki utakapochezwa, kila mtu lazima ainame na aabudu sanamu ya dhahabu. Atakayekataa kuabudu sanamu atatupwa ndani ya tanuru ya moto."

Mfalme Nebukadreza alikasirika sana sana. Alifanya tanuru ikawa moto mara saba zaidi ya kawaida. Wanajeshi wake wa nguvu walifunga Shadraka, Meshaki na Abednego. Wanajeshi waliwatupa ndani ya tanuru ya moto. Tanuru ilikuwa moto sana hatu ilichoma na kuua wale wanajeshi walipoikaribia. Shadraka, Meshaki na Abednego walianguka ndani ya tanuru ya moto.

Mfalme Nebukadreza aliangalia ndani ya tanuru. Alistuka alipoona watu wanne wakitembea katikati ya moto. Nebukadreza aliruka juu. Akauliza watumishi wake, "Hatukufunga watu watatu na kuwatupa ndani ya tanuru ya moto?" Watumishi walijibu, "Ndiyo, Ee Mfalme." Nebukadreza alisema, "Angalia! Ninaona watu wanne wanatembea ndani ya moto. Hawajafungwa. Hawajaumizwa kwa moto. Mtu wa nne anaonekana kama malaika."



Mfalme Nebukadreza aliita kwa sauti, "Shadraka, Meshaki na Abednego, watumishi wa Mungu mmoja wa kweli. Kuja nje! Kuja hapa!" Shadraka, Meshaki na Abednego walitembea na kutoka kwa tanuru ya moto. Hawakuwa wamechomeka. Nguo na nywele zao hazikuwa zimeungua. Hawakuwa na harufu ya moto. Hawakuwa wameumia. Mungu alikuwa ametuma malaika awaokoa kutoka kwa moto.

Halafu Nebukadreza alijua kwamba Mungu ni mmoja aliye wa kweli. Mungu alikuwa ameokoa Shadraka, Meshaki na Abednego kutoka kwa tanuru ya moto. Alikuwa ni Mungu wa uwezo na wa kweli. Mfalme Nebukadreza alitoa amri mpya kwa kila mtu katika ufalme wake. Amri mpya ilikuwa kwamba mtu yeyote asizungumze kinyume juu ya Mungu wa Shadraka, Meshaki na Abednego. Nebukadreza alisema kwamba yeyote atakayesema kinyume juu ya Mungu atakatwa katwa kwa vibande.

Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa na ujasiri sana. Waliamua kutii Mungu, hata kama ni kukufa. Mungu aliokoa Shadraka, Meshaki na Abednego. Imani yao ilileta heshima kwa Mungu.

Muziki ulianza kuchezwa. Papo hapo watu wote walianguka chini. Waliabudu sanamu ya dhahabu. Watu watatu tu walibaki wamesimama. Shadraka, Meshaki na Abednego walibaki wamesimama hali watu wengine wote waliinama. Na ujasiri mkuu walitii Mungu.

Nabukadreza alikasirika sana. Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa wamemuasi. Walikataa kuabudu sanamu ya dhahabu. Nebukadreza aliwaliza, "Ni ukweli kwamba hamwezi kutumikia miungu au kuabudu sanamu ya dhahabu? Mkikataa kuabudu sanamu ya dhahabu, mtatupwa ndani ya tanuru ya moto. Mungu gani atamwokoa kutoka huko?"

Shadraka, Meshaki na Abednego walijibu Mfalme, "Mungu mwenye tunamtumikia anaweza kutuokoa kutoka kwa tanuru ya moto. Lazima tutatii Mungu hata kama tutakufa. Hatutaabudu sanamu ya dhahabu."